Find this and other free resources at:

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi* ______________

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI**

**060**

# HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI
## (MKONDO WA AMALI)

(Kwa wanafunzi Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2:30** **Mwaka: 2025**

**Maelekezo**

1. Upimaji huu una sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali **yote** kwenye nafasi ulizopewa.
3. Sehemu A ina alama **kumi na tano (15)**, sehemu B **sabini (70)** na sehemu C ina alama **kumi na tano (15)**.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu yenye wino wa **bluu au mweusi**.
5. Vifaa vyote vya mawasiliano na vitu vingine visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha upimaji.
6. Andika **Namba yako ya Upimaji** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| NAMBA YA SWALI | ALAMA | SAHIHI YA MPIMAJI |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| 7 | | |
| 8 | | |
| 9 | | |
| 10 | | |
| JUMLA | | |
| SAHIHI YA MHAKIKI | | |

2 519060 100035



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*____________

**SEHEMU A (Alama 15)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo uliyopewa na kuandika herufi yake katika kisanduku ulichopewa.

(i) Wakati wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili mwalimu aliwaonesha wanafunzi picha za majengo ya kale na sanaa za jadi. Vitu hivyo hutambulika kama:

A maeneo muhimu kwa ajili ya utalii.
B historia na utambulisho.
C urithi wa kihistoria na kiutamaduni.
D visaidizi vya kuelewa historia yetu.

(ii) Kabla ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, Zanzibar ilikuwa imepata uhuru uliojulikana kama "Uhuru wa bendera". Uhuru huo ulipatikana mwaka gani?

A 1957 B 1963
C 1961 D 1962

(iii) Serikali ya Tanganyika iliongozwa na kiongozi gani kabla ya kuwa Jamhuri mwaka 1962?

A Gavana Mkuu B Waziri Mkuu
C Rais D Malkia

(iv) Ni ipi kati ya orodha zifuatazo inabainisha nguzo ya kujenga maadili katika mfumo wa elimu ya jadi?

A Mila na desturi za jamii, ujuzi wa kazi, lugha, jando na unyago
B Jando na unyago, mavazi na mafunzo ya kusaidia vijana
C Vyakula, mila na desturi, ujuzi wa kazi za jamii na umoja
D Mila na desturi za jamii, lugha, muziki na vyakula vya jamii

(v) Ni kwa namna gani unaweza kumaliza mgogoro kati ya wanafunzi wawili wanaopigana darasani kwa kutumia maarifa ya mifumo ya haki ya jadi?

A Kumuadhibu aliyesababisha ugomvi
B Kuwatenganisha wasiendelee kupigana
C Kuwapatanisha na kumaliza ugomvi kati yao
D Kuwashitaki kwa mujibu wa sheria za shule

(vi) Wanafunzi wa shule yako walipata fursa ya kutembelea mbuga za wanyama za Serengeti na Ngorongoro. Yapi kati ya maelezo yafuatayo yanatoa maana sahihi ya shughuli hiyo?

A Kusafiri na kukaa nje ya shule kwa muda
B Kwenda nje ya shule kwa ajili ya burudani
C Kutoka shuleni kwenda mbugani kwa wanyama
D Kutoka nje ya shule yako kwa lengo la kujifunza



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(vii) Ni mbinu ipi ilitumiwa na wakoloni kudhoofisha matumizi ya tiba za jadi?
- A Kuziondoa kwenye mtaala wa shule zao
- B Kutowaajiri wakunga na matabibu wa jadi
- C Kutowapa mafunzo ya kisasa waganga wa jadi
- D Kuzihusianisha na uchawi na ushirikina

(viii) Maelezo yapi yanathibitisha ukweli kuhusu jamii zilizoamua kuungana na wavamizi wa kikoloni ili kuweza kuwashinda maadui zao wa muda mrefu?
- A Zilitawaliwa kirahisi na wakoloni
- B Ziliimarika kisiasa na kiuongozi
- C Zilifanikiwa kiuchumi na kiusalama
- D Zilipata misaada ya silaha za kivita

(ix) Ni kwa namna gani udhibiti wa rasilimali kwa watu binafsi na vikundi katika mfumo wa kikabaila ulikuza siasa za jamii husika?
- A Ulisababisha kufutwa kwa mfumo wa koo
- B Ulipunguza vitendo vya rushwa katika jamii
- C Ulichangia kuendesha uchaguzi huru na haki
- D Uliwapa watu nguvu na ushawishi mkubwa katika jamii

(x) Ni kwa namna gani matumizi ya lugha ya Kiswahili katika utengenezaji wa filamu za Kitanzania yanaweza kusaidia kukuza uchumi na ushirikiano wa kimataifa?
- A Kufikia watazamaji wengi zaidi Afrika Mashariki
- B Kuifanya iwe lugha ya kufundishia ili kuongeza wataalamu
- C Kurahisisha mawasiliano katika biashara na sanaa
- D Kuzuia matumizi ya lugha nyingine nchini



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Oanisha maelezo kuhusu uhusika wa viongozi wa makabila ya jamii za Kitanzania katika harakati za kuupinga uvamizi wa kikoloni katika **Orodha A** na majina ya viongozi husika katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika jedwali ulilopewa.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Kiongozi wa kabila la Wahehe aliyepambana na Wajerumani. | A Chifu Merere |
| (ii) Kiongozi aliyeungana na Wajerumani kupigana dhidi ya Wahehe. | B Chifu Machemba |
| (iii) Kiongozi aliyeshirikiana na Wajerumani kuuangusha utawala wa Wakibosho. | C Mangi Mandara |
| (iv) Kiongozi wa Wanyamwezi aliyepinga kuenea kwa ukoloni wa Kijerumani Tanganyika. | D Mangi Mashingia |
| (v) Kiongozi wa Wayao aliyekataa kusaini mikataba ya kilaghai ya Wajerumani. | E Chifu Mkwawa |
| | F Chifu Fundikira |
| | G Chifu Mirambo |
| | H Chifu Mangungo |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | | | | | |

## SEHEMU B (Alama 70)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Bainisha umuhimu wa kuhifadhi urithi wa asili na kiutamaduni. Toa hoja tano.

(i) ______________________________________________



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

(ii) ____________________________________________

(iii) ____________________________________________

(iv) ____________________________________________

(v) ____________________________________________

4. "Maadili yana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi." Fafanua usemi huu kwa kutumia hoja tano.

(i) ____________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) ________________________________________

(iii) ________________________________________

(iv) ________________________________________

(v) ________________________________________

5. Kwa kutumia hoja tano, eleza jinsi maarifa ya mifumo ya kisiasa na kiuchumi kabla ya ukoloni yanavyoweza kutumika kuimarisha uwajibikaji katika jamii za sasa.

(i) ________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) ______

(iii) ______

(iv) ______

(v) ______

6. Chambua hatua tano za kisiasa zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania kujenga taifa baada ya uhuru.

(i) ______



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(iii) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(iv) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(v) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

7. Tumia hoja tano kuchambua mchango wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika upatikanaji wa Uhuru wa Tanganyika.

(i) ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) __________

(iii) __________

(iv) __________

(v) __________

8. Kwa kutumia hoja tano, tofautisha elimu ya jadi na elimu ya sasa.

(i) __________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii) ______

(iii) ______

(iv) ______

(v) ______

9. Changanua vigezo vitano vya kiteknolojia vinavyotofautisha zana za zama za mawe na zana za zama za chuma.

(i) ______



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

**SEHEMU C (Alama 15)**

Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Eleza mabadiliko matano ya kisiasa yaliyoletwa na utawala wa Waingereza katika jamii za Kitanzania.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org